


# "YESU KUHANI WETU MKUU"

Salamu za asubuhi kwako. Natumai umepumzika vyema usiku.

Tunaendeleza ugunduzi wetu wa Yesu-Aliye, yaani Yesu halisi katika WAEBRANIA 7.

Mwandishi wa Kitabu cha Waebrania anatangaza: Yesu ndiye Kuhani wetu Mkuu wa kudumu na wa milele anayetuwezesha kufurahia urafiki pamoja na Muumba wetu.

Yesu ni Kuhani Mkuu wa kipekee. Yeye si kuhani chini ya Sheria ya Musa kama Haruni. Yeye ni kuhani kama Melkizedeki (tizama MWANZO 14) ambaye aliishi zaidi ya miaka 400 kabla ya Sheria iliyotolewa kwenye Mlima Sinai kuwako. Kwa sababu hiyo, Yesu ni Kuhani Mkuu kuliko makuhani wengine wote.

WAEBRANIA 7:1-3: '*Huyo Melkisedeki alikuwa mfalme wa Salemu, na kuhani wa Mungu Mkuu. Abrahamu alipokuwa anarudi kutoka vitani ambako aliwaua wafalme, Melkisedeki alikutana naye, akambariki, naye Abrahamu akampa sehemu moja ya kumi ya vitu vyote alivyokuwa navyo. (Maana ya kwanza ya jina Melkisedeki ni "Mfalme wa Uadilifu;" na, kwa vile yeye alikuwa mfalme wa Salemu, jina lake pia lina maana ya "Mfalme wa Amani.") Baba yake na mama yake hawatajwi, wala ukoo wake hautajwi; haisemwi alizaliwa lini au alikufa lini. Anafanana na Mwana wa Mungu, na anaendelea kuwa kuhani daima*.'

Melkizedeki alimbariki Abrahamu akionyesha kuwa alikuwa mkuu kuliko Abrahamu.

WAEBRANIA 7:4: '*Basi, mwaona jinsi mtu huyu alivyokuwa maarufu. Babu Abrahamu alimpa sehemu moja ya kumi ya vitu vyote alivyoteka nyara vitani.*'

Melkizedeki ndiye kielelezo cha Yesu ambaye ni Kuhani Mkuu wa agano jipya na lililo bora zaidi – Yesu Kuhani Mkuu mkamilifu ambaye huwaleta Watu wa Mungu kwenye ukamilifu (tizama WAEBRANIA 7:11-12).

WAEBRANIA 7:22(nusu ya mwisho)-25: 'Kutokana na ukuhani wa Walawi, watu wa Israeli walipewa sheria. Sasa, kama huduma ya Walawi ingalikuwa kamilifu, hapangekuwa tena na haja ya kutokea ukuhani mwingine tofauti, na ambao umefuata utaratibu wa ukuhani wa Melkisedeki, na si ule wa Aroni. Maana ukuhani ukibadilika, ni lazima sheria nayo ibadilike.'

Kwa hiyo hii ina maana gani kwetu na kwa watu tunaowahudumia?

• Inamaanisha tunaweza kuokolewa kwa sababu Yesu – ambaye anaishi ili kutuombea – ndiye mpatanishi wetu, msamaha wa Baba na wokovu kwa kila mmoja wetu.
• Inamaanisha kwamba tunaweza kuishi kwa amani tukiwa marafiki wa Mungu.
• Inamaanisha kwamba tunaweza kumkaribia Mungu kila siku ili kutoa ibada na maombi yetu kwake.

Kuna mengi zaidi katika WAEBRANIA 7-8. Unaweza kutaka kusoma sura hizo kwa ukaribu.

**MUHTASARI**

Mungu amefanya jambo la kustaajabisha kutupatia Yesu kama Kuhani wetu Mkuu mkamilifu, wa milele. Jambo hili lilichukua muda wa miaka 2000 ili lifanyike sahihi, na baada ya kufufuka kwake Yesu, Mungu akampa kwetu kuwa Kuhani Mkuu.

**MASWALI**

- Je, unaamini kwamba Yesu anaweza kukupa uwezo wa kumfikia Baba kwenye msingi wa kirafiki?
- Ikiwa unaamini hili, unatumiaje fursa hii ya kustaajabisha?
- Na hili lina maana gani kwa maisha yako ya baadaye?

Juma Lijalo: Yesu anasema nini kuhusu yeye mwenyewe?

Ubarikiwe sana katika jina la Yesu.



Douglas Van Devender.
Huduma za 'Jesus Ministries International' na 'Transforming Prayer'.

**TANGAZO LA KUZINGATIA:**
Wengine wanaweza kuongezwa kwenye orodha yetu ya barua-pepe kwa kutuma majina yao, eneo na barua pepe kwa
WDV2023@outlook.com
(Mtu yeyote anaweza kujiondoa kwa kutuma neno STOP kwa anwani sawa ya barua pepe.) Ahsante.